ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Kipindi cha Nusu Mwaka 2021/22 na Mwelekeo Wake kwa Nusu ya Pili*

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2022**

ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

***Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Kipindi cha***

***Nusu Mwaka 2021/22 na Mwelekeo Wake kwa Nusu ya Pili***

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2022**

## Utangulizi

Tamko la Sera ya Fedha lililotolewa mwezi Juni 2021 liliweka bayana malengo ya Benki Kuu ya Tanzania ya utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2021/22 yanayoendana na malengo mapana ya Serikali katika kuendeleza utulivu wa mfumuko wa bei na kusaidia ukuaji endelevu wa uchumi. Taarifa hii ya mapitio ya nusu mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha la mwaka 2021/22, inatoa tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa Tanzania, na kuonesha mwenendo wa utekelezaji wa malengo ya sera ya fedha na matokeo yake katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 kama yalivyoanishwa katika Tamko la Sera ya Fedha la mwezi Juni 2021. Vilevile, taarifa hii inatoa mwelekeo wa uchumi wa Tanzania, pamoja na sera ya fedha katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2021/22 ili kuwezesha kufikia malengo ya kuendelea kuwa na mfumuko mdogo wa bei na kusaidia kukuza uchumi.

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha Katika Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2021/22

Katika mwaka 2021/22, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakiksha uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kwenye uchumi kwa ajili ya mabenki kukopesha sekta binafsi. Utekelezaji huu ulikusudia kufikia lengo la ukuaji wa Pato la Taifa la asilimia 5.6 kwa mwaka 2021 na kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 3-5. Ili kutimiza malengo haya, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

i. ukuaji wa fedha taslimu wa asilimia 9.9;
ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;
iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.6; na
iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021/22, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwenye uchumi kama ilivyoainishwa kwenye Tamko la Sera ya Fedha la mwaka 2021/22. Lengo kuu ni kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ili kufufua shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na janga la UVIKO-19. Ili kufanikisha lengo hili, Benki Kuu ya Tanzania ilitumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha kwa ajili ya kuongeza ukwasi katika sekta ya benki, ikiwemo kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki, kununua fedha za kigeni kwenye soko la jumla la fedha za kigeni, na kuingia mikataba ya kubadilishana fedha za kigeni na mabenki. Vilevile, Benki Kuu ilichukua hatua za ziada za kisera kwa ajili ya kuchochea ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi ambazo ni:

(i) kuanzishwa kwa mfuko maalum wa shilingi trilioni moja kwa ajili ya kukopesha mabenki na taasisi za fedha kwa riba ya asilimia 3, ili zitoe mikopo kwa sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka;

(ii) kupunguza kiwango cha sehemu ya amana za mabenki

kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu kisheria kwa benki itakayotoa mikopo kwa sekta ya kilimo kulingana na kiasi cha mkopo kitakachotolewa kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka;

(iii) kulegeza masharti ya usajili wa mawakala wa benki kwa kuondoa sharti la kuwa na uzoefu wa kufanya biashara wa angalau miezi 18 na badala yake waombaji wa biashara ya wakala wa benki watatakiwa kuwa na kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho wa Taifa kutoka NIDA;

(iv) kuweka ukomo wa kiwango cha riba kinachotolewa kwenye akaunti za wateja wa makampuni ya watoa huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi kwa kuhakikisha kuwa riba inayotolewa kwa ajili ya amana hizi haizidi riba inayotolewa na benki husika kwa amana za akiba (*saving deposit rate*);

(v) kupunguza kiwango cha mtaji kinachotakiwa kuwekwa na benki za biashara kwa ajili ya kuwezesha kutoa mikopo.

Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza chachu ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza viwango vya riba.

Utekelezaji wa sera ya fedha ulisaidia kudumisha kiwango cha kutosha cha ukwasi katika sekta ya benki, kwa ajili ya kuchochea utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kuwezesha ufanyaji wa miamala ya malipo kwa ufanisi. Hali hii iliakisiwa na utulivu wa riba katika masoko ya fedha, uwepo wa amana za kutosha za mabenki katika Benki Kuu ya Tanzania na ongezeko la ukuaji wa ujazi wa fedha. Mathalani, riba ya siku moja katika soko la fedha baina

ya mabenki ilikuwa ni wastani wa asilimia 3.85 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021, sawa na wastani wa kipindi kama hicho mwaka 2020. Vilevile, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi ilibakia katika wastani wa asilimia 4. Wastani wa fedha taslimu uliongezeka kwa asilimia 10.1 ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 9.9, wakati ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 12.9, ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 10. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuongezeka kufikia wastani wa asilimia 5.9, ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 10.6 kwa mwaka 2021/22. Aidha, katika kipindi cha mwaka ulioishia Desemba 2021, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliongezeka kwa kasi nzuri zaidi na kufikia asilimia 10.0.

Viwango vya riba za mikopo ya mabenki viliendelea kupungua japo kwa kasi ndogo. Hali hii inatokana na kuchelewa kuonekana kwa matokeo ya hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu, pamoja na kiwango cha juu cha tahadhari kinachochukuliwa na mabenki katika utoaji wa mikopo, hususan kufuatia athari za UVIKO-19 kwa biashara na uwekezaji na vikwazo vingine vya kimfumo. Kutokana na changamoto hizi, riba za mikopo zilibakia katika wastani wa asilimia 17.

**Mwenendo wa Uchumi wa Dunia**

Uchumi wa dunia uliendelea kuimarika kutoka katika athari za janga la UVIKO-19, katika robo ya pili na ya tatu ya mwaka 2021 kufuatia hatua zilizochukuliwa za utekelezaji wa sera wezeshi ya fedha na

bajeti ili kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi, pamoja na kupunguza makali ya masharti yaliyokuwa yamewekwa kwa lengo la kuzuia kusambaa kwa virusi vya UVIKO-19. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi ilikuwa ndogo kuliko ilivyotarajiwa kutokana na kuibuka kwa aina mpya ya virusi vya UVIKO-19, pamoja na mikwamo kwenye minyororo ya ugavi duniani. Kutokana na mwenendo mzima wa uchumi wa dunia, taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Januari 2022 ilitoa makisio ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2021 kuwa asilimia 5.9. Aidha, IMF ilirekebisha makadirio ya ukuaji kwa mwaka 2022 kuwa asilimia 4.4 kutoka makadirio ya awali ya asilimia 4.9 kutokana na kushuka kwa makadirio ya ukuaji wa nchi mbili kubwa duniani—Marekani na China.

Ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kuwa asilimia 3.7 kwa mwaka 2022 na asilimia 4.0 kwa mwaka 2023. Ukuaji wa uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na zile za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) unatarajiwa kufikia asilimia 4.9 na asilimia 3.9 kwa mwaka 2021, kutoka matarajio ya awali ya asilimia 5.7 na asilimia 2.7, mtawalia. Aidha, taarifa ya Benki ya Dunia ya mwezi Januari 2022 inakadiria uchumi wa dunia kukua kwa asilimia 5.5 mwaka 2021 kutokana na kulegezwa kwa masharti ya kufungia shughuli za kiuchumi katika nchi nyingi. Uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 4.1 kwa mwaka 2022 kutokana na kuendelea kuwepo kwa janga la UVIKO-19 na kupungua kwa misaada ya kifedha inayotolewa kwa ajili ya kunasua shughuli za kiuchumi na mikwamo kwenye ugavi.

Uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.6 mwaka 2022 kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa kufuatia kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika nchi washirika wa kibiashara.

Mfumuko wa bei uliongezeka katika nchi nyingi duniani kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa na mikwamo katika ugavi. Ongezeko la mfumuko wa bei lilionekana zaidi katika nchi za Marekani, Umoja wa nchi za Ulaya na Uingereza. Aidha, mfumuko wa bei katika nchi za China na India uliongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji sambamba na mikwamo ya minyororo ya ugavi. Mfumuko wa bei katika nchi nyingi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliongezeka kidogo, japo ulibakia ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa asilimia 8.0. Ongezeko hili kwa kiwango kikubwa lilitokana na kupanda kwa bei za vyakula, usafiri na mafuta. Wakati huohuo, viwango vya mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) vilibaki ndani vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa asilimia 3-7, isipokuwa kwa nchi za Zambia, Zimbabwe, Shelisheli, Angola, Malawi na Botswana. Ongezeko la mfumuko wa bei katika nchi hizi lilitokana na kupanda kwa bei za chakula, nishati na kuporomoka kwa thamani ya sarafu.

Aidha, kwa mujibu wa Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Januari 2022, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa juu katika nchi nyingi duniani kufuatia ongezeko la bei za vyakula na

athari za kupanda kwa bei za mafuta duniani. Mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea unatarajiwa kuwa asilimia 3.9 mwaka 2022, kabla ya kupungua hadi kufikia asilimia 2.1 mwaka 2023. Wakati huohuo, katika nchi zinazoibukia kiuchumi mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa asilimia 5.9 mwaka 2022 na kushuka hadi kufikia asilimia 4.7 mwaka 2023. Katika nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa asilimia 8.6 kwa mwaka 2022 kabla ya kupungua hadi kufikia asilimia 7.1 kwa mwaka 2023.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### *Tanzania Bara*

Uchumi umeendelea kuimarika kutoka katika athari za janga la UVIKO-19, kufuatia kufunguka kwa uchumi wa dunia na hatua zilizochukuliwa kufufua shughuli za kiuchumi. Uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 4.9 katika kipindi cha robo tatu za kwanza za mwaka 2021, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, uchimbaji madini, uzalishaji viwandani, uchukuzi na uhifadhi, na biashara. Aidha, shughuli za uchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na habari na mawasiliano, uchimbaji madini na huduma za jamii (hususan umeme na maji). Shughuli za malazi na migahawa ambazo zilikuwa na ukuaji hasi katika robo tatu za kwanza za mwaka 2020, zilikua kwa wastani wa asilimia 6, ikiwa ni ishara ya kuimarika kutoka kwenye athari za UVIKO-19.

Mfumuko wa bei umeendelea kubaki ndani ya malengo ya nchi pamoja na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi vya kikanda[1], japo umekuwa ukiongezeka katika miezi ya hivi karibuni. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa ni asilimia 4, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulitokana na kupanda kwa bei za baadhi ya vyakula na bidhaa zisizo za chakula. Mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula visivyochakatwa na nishati, ambao unabeba sehemu kubwa katika fahirisi za bei za bidhaa, ulikuwa wastani wa asilimia 4.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, kufuatia ongezeko la bei za mavazi, vifaa vya ujenzi, usafiri na kodi za makazi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3-5 katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2021/22 kufuatia matarajio mazuri ya upatikanaji wa chakula, utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za washirika wetu wa kibiashara, pamoja na utekelezaji thabiti wa sera za fedha na bajeti. Aidha, kuendelea kuongezeka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na hatari ya kuwepo kwa hali ya ukame kwa baadhi ya sehemu za nchi, zinaweza kusababisha mfumuko wa bei kuongezeka zaidi ya lengo.

Ujazi wa fedha umeendelea kukua kwa kasi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021/22 kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi.  Ukuaji wa ujazi wa

---

1 Malengo ya nchi ya mfumuko wa bei kwa mwaka 2021/22 ni wigo wa asilimia 3 hadi 5, ukomo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni asilimia 8 na kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ni wigo wa asilimia 3 hadi 7.

fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 12.9 ukilinganishwa na asilimia 7.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji wa M3 kinaendana na lengo la wastani wa ukuaji wa asilimia 10 kwa mwaka 2021/22. Wastani wa ukuaji wa fedha taslimu uliongezeka na kufikia asilimia 10.1 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, kiwango ambacho kinaendana na lengo la ukuaji wa asilimia 9.9 kwa mwaka 2021/22. Sambamba na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika uchumi, na mwenendo wa kuridhisha wa ukuaji wa ujazi wa fedha, kuna matarajio makubwa ya kufikia malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2021/22.

Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 5.9 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021, ukilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, kiwango ambacho ni kidogo kikilinganishwa na lengo la wastani wa asilimia 10.6 kwa mwaka 2021/22. Kasi ndogo ya ukuaji mikopo kwa sekta binafsi ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya mikopo mipya kutokana na athari za janga la UVIKO-19 kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi. Aidha, kasi ya ukuaji wa mikopo kwa miezi ya hivi karibuni imeanza kuongezeka na kufikia kiwango cha asilimia 10.0 mwezi Desemba 2021, sambamba na hatua za kisera zilizochukuliwa na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi. Kiwango kikubwa cha mikopo kilielekezwa kwenye shughuli binafsi (shughuli ndogondogo na shughuli za kati), biashara, na uzalishaji viwandani. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa

kuendelea kuimarika katika nusu ya pili ya mwaka 2021/22, kufuatia utekelezaji wa sera wezeshi ya fedha, kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia.

Shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa imara dhidi ya sarafu nyingine za washirika wetu wa kibiashara katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021/22. Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,308.30 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,309.19 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, ikiwa ni sawa na ongezeko la thamani kwa wastani wa asilimia 0.04. Kuimarika kwa thamani ya shilingi kulichangiwa zaidi na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei nchini, uwepo wa kiwango cha kutosha cha akiba ya fedha za kigeni na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti. Aidha, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani inatarajiwa kuendelea kuwa imara na tulivu katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2021/22.

Mwenendo wa utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021 ulikuwa wa kuridhisha, kufuatia kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya kodi, hali iliyochangiwa na kuendelea kuimarika kwa uchumi pamoja na jitihada za Serikali kusimamia ukusanyaji wa mapato. Ukusanyaji wa mapato ya ndani (mapato ya kodi na yasiyo ya kodi) ulifikia shilingi bilioni 11,837.0 ikiwa sawa na asilimia 90.7 ya lengo la makusanyo kwa kipindi husika. Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 10,507.9, ambapo kiwango kikubwa kilikusanywa kupitia kodi ya mapato ya mashirika na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa bidhaa zinazotoka nje. Aidha, marejesho katika kodi ya ongezeko la thamani yalikuwa kiasi cha

shilingi bilioni 601.7. Matumizi ya Serikali yaliendelea kufanyika kuendana na kiwango cha mapato huku kipaumbele kikiwa katika kutekeleza miradi itakayowanufaisha zaidi wananchi wenye kipato cha chini ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya afya, maji na elimu ikijumuisha miradi ya kimkakati. Katika kipindi hiki, matumizi ya Serikali yalikuwa ni shilingi bilioni 15,034.7 sawa na asilimia 90.8 ya makadirio, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa ni asilimia 56.5.

Deni la ndani na nje la Serikali lilifikia dola za Marekani milioni 29,746.9 kutoka dola milioni 28,011.2 mwishoni mwa mwezi Juni 2021, ambapo deni la nje likiwa ni asilimia 75.6. Tathmini ya uhimilivu wa deni la taifa iliyofanyika mwezi Novemba 2021 inaonesha kuwa deni la ndani na nje la Serikali limeendelea kuwa himilivu, na thamani yake kwa sasa ni asilimia 31 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55.

Sekta ya nje imeendelea kuimarika kutoka kwenye athari ya janga la UVIKO-19, kufuatia kuendelea kufunguka kwa uchumi wa dunia na shughuli za utalii. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021, mapato yanayotokana na shughuli za utalii yaliongezeka, japo yamebakia chini ya kiwango kilichorekodiwa kabla ya janga la UVIKO-19, hali inayoashiria kuendelea kuimarika kwa shughuli za utalii. Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje ilikuwa dola za Marekani milioni 962.1, kutoka dola milioni 380.0 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2020, kutokana na kuongezeka zaidi kwa uagizaji bidhaa za mashine, vifaa vya ujenzi na mafuta kutoka nchi za nje. Uagizaji wa bidhaa na huduma ulifikia

dola za Marekani milioni 6,574.5 kutoka dola za kimarekani milioni 4,699.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 24.7 na kufikia dola za Marekani milioni 5,735.0 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021, kutokana na ongezeko la mapato ya huduma nje ya nchi na mauzo ya bidhaa zisizo asilia. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kubaki katika viwango vya kuridhisha kukidhi mahitaji ya nchi kutoka nje ya nchi na kufikia dola za Marekani milioni 6,386.0 mwishoni mwa mwezi Desemba 2021. Kiasi hiki kinatosha kulipia uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takriban miezi 6.6, kiwango ambacho kinaendana na lengo la nchi la kuwa na akiba isiyopungua miezi minne na kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha kuwa na angalau miezi minne na nusu, na angalau miezi sita kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Sekta ya benki imeendelea kuwa imara, yenye mtaji na kiwango cha ukwasi cha kutosha. Ubora wa rasilimali za mabenki uliimarika kufuatia kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu hadi asilimia 8.2 ya mikopo yote mwezi Desemba 2021, kutoka asilimia 9.3 mwezi Juni 2021. Hata hivyo, uwiano huu bado uko juu ya kiwango kinachokubalika cha angalau asilimia 5. Aidha, benki zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kutatua changamoto ya mikopo chechefu ikiwemo kuimarisha ufuatiliaji wa vihatarashi vya kiusimamizi, pamoja na kuboresha vigezo vinavyotumika katika kuidhinisha mikopo mipya ikiwemo matumizi ya taarifa za wakopaji kutoka kwenye kanzidata ya taarifa za wakopaji. Vilevile, Benki Kuu

inaendelea kuhimiza benki kuweka mikakati kwa ajili ya kupunguza mikopo chechefu, ikiwemo kuzitaka benki kuwasilisha taarifa zao za mikopo kwenye kanzidata ya taarifa za wakopaji. Benki Kuu itaendelea kusimamia maadili ya kiutendaji ya watumishi wa benki na kusisitiza kufuata miongozo ya kiutendaji kama ilivyoainishwa na Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA).

Mifumo ya malipo imeendelea kuimarika na kufanya kazi kwa ufanisi, kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kidigitali katika kufanya miamala. Mafanikio makubwa yalionekana katika uimarishwaji wa upatikanaji wa huduma za fedha kupitia simu za mkononi; ambapo idadi ya watu wazima wanaotumia huduma za fedha kupitia simu zao za mkononi ilifika asilimia 80.3 mwezi Desemba 2021, ikilinganishwa na asilimia 78.7 mwezi Juni 2021. Kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi katika huduma za fedha nchini Tanzania kumerahisisha na kuboresha utoaji wa huduma jumuishi za fedha kwa makundi yasiyofikiwa na huduma rasmi za kibenki, ikilinganishwa na njia nyingine katika upatikanaji wa huduma rasmi za fedha. Maendeleo haya yamejidhihirisha katika kuongezeka kwa matumizi ya huduma za kifedha kupitia simu za mkononi ambayo yalifikia asilimia 94.3 kwa mwezi Desemba 2021 kutoka asilimia 93.2 mwezi Juni 2021. Pia, maamuzi ya kisera ya Benki Kuu ya kuongeza ukomo wa kiwango cha miamala ya fedha kupitia simu za mikononi wakati wa kupambana na janga la UVIKO-19 yamechangia kuongezeka kwa matumizi ya huduma za fedha kidigitali.

Vilevile, Benki Kuu imekamilisha uundwaji wa Mfumo wa Malipo ya Papo Hapo Nchini (*Tanzania Instant Payment System*) ambao uko katika hatua ya majaribio. Mfumo huu utarahisisha na kuboresha muingiliano baina ya mifumo tofauti ya malipo nchini, kwa kuunganisha watoa huduma za malipo waliosajiliwa (benki na wasio benki) ili kuwezesha ukamilishaji/ufanyaji wa miamala ya malipo kwa urahisi, haraka, gharama nafuu na kwa usalama. Kukamilika kwa mfumo huu kutakuwa na faida nyingi za kiuchumi zikiwemo kuhamasisha ongezeko la matumizi ya huduma za fedha kidigitali katika jamii, kuongeza miamala, kupunguza matumizi ya fedha taslimu, kuboresha usimamizi wa sekta ya fedha na kuchochea huduma jumuishi za fedha.

***Zanzibar***

Uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika kutoka kwenye athari za janga la UVIKO-19, kufuatia hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kufunguka kwa uchumi wa dunia. Katika kipindi cha robo tatu za kwanza za mwaka 2021, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 5.8, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huu ulitokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, hususan zile zinazohusiana na utalii, kama malazi na huduma za chakula. Aidha, shughuli za uchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na malazi na huduma za chakula, utawala, umeme, afya na huduma za jamii, fedha na bima.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa katika viwango vya chini na tulivu, ndani ya lengo la ukomo wa asilimia 5, japo umeongezeka kidogo. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 2.2, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.9 katika kipindi kama hicho kwaka 2020. Ongezeko hili lilitokana na kupanda kwa bei za bidhaa zisizohusisha chakula kufikia wastani wa asilimia 3.8, kutoka asilimia 0.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, kutokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa za mafuta[2]. Aidha, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya lengo katika nusu ya pili ya mwaka 2021/22, kutokana na kuimarika kwa mnyororo wa ugavi katika soko la dunia.

Utekelezaji wa shughuli za kibajeti katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021 ulikuwa wa kuridhisha kufuatia kuongezeka kwa mapato ya serikali kutokana na kuimarika kwa shughuli za utalii na jitihada za Serikali katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato. Makusanyo ya kodi yalifikia asilimia 72.8 ya lengo, wakati makusanyo yasiyo ya kodi yalikuwa asilimia 73.8 ya lengo. Katika kipindi hicho, jumla ya matumizi yalikuwa shilingi bilioni 465.6, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 368.0. Deni la Serikali liliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 897.5 mwishoni mwa mwezi Desemba 2021, kutoka shilingi bilioni 887.0 mwishoni mwa mwezi Juni 2021, ambapo asilimia 77.5 lilikuwa ni deni la nje.

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje ilipungua hadi dola za Marekani milioni 92.8 katika

2 Bidhaa za mafuta zinajumuisha petroli, dizeli na mafuta ya taa

kipindi cha Julai hadi Desemba 2021, kutoka nakisi ya dola za Marekani milioni 153.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kupungua huku kulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, pamoja na kupungua malipo kwa ajili ya uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 118.9 kutoka dola za kimarekani milioni 46.5, hali iliyochangiwa zaidi na kuongezeka kwa mapato yanayotokana na shughuli za utalii na mauzo ya karafuu. Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi ulipungua kwa asilimia 11.0 hadi dola za Marekani milioni 224.7, kutoka kiwango kilichorekodiwa mwaka 2020, kutokana na kupungua kwa uagizaji mashine na vifaa vya uchukuzi.

**Mwelekeo wa Uchumi**

Uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kuimarika kadri changamoto zitokanazo na mikwamo katika upande wa minyororo ya ugavi zinavyopungua, sambamba na matarajio ya kupungua kwa athari za UVIKO-19. Aidha, kuongezeka kwa upatikanaji wa chanjo katika nchi nyingi kunatarajiwa kuimarisha biashara na uwekezaji duniani. Matarajio haya yanaweka mazingira mazuri kwa ajili ya ukuaji wa uchumi wa ndani ambao umeendelea kuimarika. Uchumi wa Tanzania bara unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.0 mwaka 2021, badala ya makadirio ya awali ya asilimia 5.6 kutokana na athari za UVIKO-19, japo ukuaji unatarajiwa kuongezeka katika vipindi vinavyofuata. Katika mwaka 2022, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.2 kutokana na uwekezaji unaoendelea kufanywa

na Serikali na sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu, usafiri, maliasili, viwanda na kilimo. Uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2021 na asilimia 6.4 kwa mwaka 2022. Ukuaji huu utachangiwa na utekelezaji wa mipango ya Serikali katika kuboresha uchumi wa bluu na kuimarika kwa biashara za utalii. Utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi na sera madhubuti ya bajeti, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara vitasaidia kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa Tanzania bara na Zanzibar. Hata hivyo matarajio haya yatategemea sana na kupungua kwa athari za janga la UVIKO-19.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya wigo wa asilimia 3-5 na chini ya asilimia 5 katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2021/22 kwa Tanzania bara na Zanzibar, mtawalia. Matarajio haya yatachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa chakula cha kutosha katika maeneo mengi nchini, utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu nyingine duniani na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti. Aidha, athari zitokanazo na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia na kutokuwepo kwa mvua za kutosha katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka hapa nchini inaweza kusababisha mfumuko wa bei kuongezeka zaidi ya lengo.

Sekta ya fedha inatarajiwa kuimarika kwa kiwango kikubwa kufuatia kuimarika kwa shughuli za biashara na uwekezaji duniani na maboresho yanayoendelea kutekelezwa katika sekta ya fedha,

pamoja na kuongezeka kwa ubunifu katika utoaji wa huduma za fedha hususan kupitia matumizi ya teknolojia. Vilevile, hatua zinazochukuliwa katika kuongeza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza viwango vya riba, pamoja na kuboresha mazingira ya kibiashara na kupunguza mikopo chechefu inatarajia kusaidia kuimarisha zaidi sekta ya fedha. Hatua hizi zitachangia kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi, usimamizi rasilimali, na ufanisi wa utoaji wa huduma za fedha. Pia, maendeleo haya yataboresha utekelezaji wa sera ya fedha na kusaidia kufikia malengo mapana ya Serikali ya kuwa na mfumuko mdogo wa bei na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

## Mwelekeo wa Sera ya Fedha katika Kipindi cha Nusu ya Pili ya Mwaka 2021/22

Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi katika uchumi ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kupitia ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza gharama za mikopo. Utekelezaji huu utafanyika kuendana na matarajio ya mfumuko mdogo wa bei wa kati ya asilimia 3-5 kwa Tanzania bara na chini ya asilimia 5 kwa Zanzibar. Benki Kuu itaendelea kutumia nyenzo mbalimbali katika kutekeleza sera ya fedha ili kufikia malengo yanayotarajiwa. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kuboresha masoko ya fedha ili kuongeza ufanisi wa sera ya fedha. Aidha, Benki Kuu itaimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ukwasi katika sekta ya benki kwa lengo la kuhakikisha utulivu wa hali ya ukwasi,

na kupungua kwa viwango vya riba za mikopo na kiwango cha mikopo chechefu. Benki Kuu pia itaongeza uwazi kwa kuboresha mawasiliano kuhusu utekelezaji sera ya fedha na mwenendo wa hali ya uchumi na kushirikiana na wadau katika kutatua changamoto za kimfumo na za kiusimamizi katika sekta ya fedha.

**Hitimisho**

Uchumi wa dunia unaendelea kuimarika kutoka kwenye athari za UVIKO-19, na matarajio kwa mwaka 2022 yanatia matumaini, licha ya changamoto za kuibuka kwa aina mpya ya virusi vya ugonjwa wa UVIKO-19 na mikwamo katika minyororo ya ugavi. Pia, matarajio ya ukuaji wa uchumi wa ndani yana mwelekeo chanya, yakichagizwa na maendeleo mazuri ya kuimarika kwa shughuli za kiuchumi yaliyoonekana hivi karibuni, uwekezaji unaofanywa na Serikali zote mbili na sekta binafsi, pamoja na utekelezaji wa sera wezeshi na hatua zinazochukuliwa kuunasua uchumi kutoka kwenye athari za UVIKO-19. Kutokana na mwelekeo huu, makadirio ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania bara wa asilimia 5 kwa mwaka 2021 na asilimia 5.2 kwa mwaka 2022, na kwa Zanzibar, ukuaji wa asilimia 5.2 na asilimia 6.4, mtawalia, yanategemewa kufikiwa. Mfumuko wa bei kwa Tanzania bara na Zanzibar unatarajiwa kubakia ndani ya malengo yaliyowekwa katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2021/22 na hivyo kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika uchumi na hivyo kuchochea ukuaji wa biashara na uwekezaji.

Ili kuchangia ukuaji endelevu wa uchumi sambamba na matarajio ya utulivu wa bei, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwenye uchumi katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2021/22. Msisitizo mkubwa utaendelea kuwekwa katika kuboresha ufanisi wa sera ya fedha na kuondoa vikwazo vinavyozuia ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupungua kwa viwango vya riba. Utekelezaji huu wa sera wezeshi ya fedha pamoja na hatua zinazochukuliwa katika kusimamia sekta ya fedha, maboresho ya mazingira ya biashara pamoja na sera madhubuti ya bajeti vitasaidia kuimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi. Kwa muktadha huu, ni matarajio ya Benki Kuu ya Tanzania kuwa malengo ya sera ya fedha yaliyowekwa katika Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2021/22 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328/9, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz